*Namba ya Mtahiniwa*________________________
*Jina la Shule* ________________________________
*Mkoa*_______________________________________
*Wilaya*_______________________________________


# KEYS EDUCATIONAL AND STATIONERY SERVICES (KESS)
## NAMBA YA USAJILI: 473801

Barua pepe: keyseducationalservices@gmail.com
**Simu: 0758587618/0679587618**
**KIFURU-KINYEREZI, DAR ES SALAAM**


# MTIHANI WA UKARIBISHO DARASA LA SABA 2025
## 01: KISWAHILI

**Muda: Saa 1:Dakika 40 ______________________Februari 20, 2025**

**Maelekezo**

1. Mtihani huu una sehemu **A, B,** na **C** zenye jumla ya maswali **sita (6)**
2. Jibu maswali **yote** katika kila sehemu
3. Majibu yote yaandikwe katika karatasi hii
4. Tumia kalamu ya wino wa rangi ya **buluu** au **mweusi**
5. Simu za mikononi na vifaa vingine visivyohitajika **haviruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
6. Andika kwa usahihi **Jina lako** na **Jina la Shule** sehemu ya juu kulia kwenye kona ya kila ukurasa

| KWA MATUMIZI YA MTAHINI TU | | |
|---|---|---|
| **NAMBA YA SWALI** | **ALAMA** | **JINA LA MTAHINI** |
| 1. | | |
| 2. | | |
| 3. | | |
| 4. | | |
| 5. | | |
| 6. | | |
| **JUMLA** | | |
| **SAINI YA MWINGIZA ALAMA** | | |
| **SAINI YA MHAKIKI** | | |

**SEHEMU A (Alama 20)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Sikiliza kwa makini hadithi utakayosomewa na msimamizi, kisha jibu kipengele cha (i) – (v), **kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi** na kuandika katika kisanduku.

(i) Busara na bibi yake wanaishi katika kijiji gani?
A. Tumaini C. Tuliani E. Mkomazi
B. Matumaini D. Mwendokasi

(ii) Kijiji wanachoishi Busara na Bibi yake kipo karibu na nini?
A. Msitu wa Mkomazi C. Shule ya Msingi Tumaini E. Mto Mkomazi
B. Hifadhi ya Wanyama ya Mkomazi D. Kijiji cha Mwendokasi

(iii) Busara anasoma katika shule gani?
A. Tumaini C. Tuliani E. Mkomazi
B. Matumaini D. Mwendokasi

(iv) Busara aliona wanyama gani?
A. Ng'ombe C. Tembo E. Simba
B. Pundamilia D. Twiga

(v) Nahau kupigwa na butwaa kama ilivyotumika katika habari uliyoisikiliza ina maana gani?
A. Kupatwa na mshangao C. Kuwa na huruma E.Kutamani kitu
B. Kuwa tayari kwa jambo lolote D. Kusubiri kitu kwa hamu

2. Kuanzia swali la (i)-(x), chagua jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kisanduku.

(i) Zawadi a<u>li</u>safiri siku nzima kutoka Songea kwenda Arusha. Silabi iliyopigiwa mstari inawakilisha nini?
A. Njeo C. Nafsi E. Hali
B. Awali D. Ukanushi

(ii) Baada ya kukimbia mbio ndefu____________ kwa uchovu. Neno lipi linakamilisha sentensi hii?
A. Alitweta C. Aliteta E. Alipweta
B. Alitweka D. Alitwetwa

(iii) Hatupaswi kuwaonea wenzetu gere au wivu kutokana na majaliwa yao, kila mtu amejaliwa jaala au majaliwa yake. Maelezo haya yana maana sawa na methali ipi kati ya hizi zifuatazo?
A. Baniani mbaya kiatu chake dawa D. Jumbe ni watu si kilemba
B. Mjaliwa ni mmoja, kila mtu ana lake E. Mvuvi ndiye ajuaye pweza alipo
C. Mambo ni kangaja, huenda yakaja

(iv) Ndege asiyenaswa leo______________. Kifungu kipi kinakamilisha methali hii?
A. Ni kitoweo cha kesho C. Hawezi kunaswa tena E. Hukamatwa na ulimbo
B. Harudi tena kwenye mtego D. Mtego wake ni mbovu

(v) Baba alisema, "Nitakusomesha mwakani." Kauli taarifa ya sentensi hii ni ipi?
A. Baba alisema kwamba nitakukomesha mwakani
B. Baba alisema kwamba atanisomesha mwakani
C. Baba alisema kwamba angenisomesha mwaka unaofuata
D. Baba alisema kwamba hatanisomesha mwakani
E. Baba alisema kwamba ningekusomesha mwaka ule

(vi) Mtoto mwema ni yule asiyependa <u>shari</u> na wenzake. Neno lipi kati ya haya yafuatayo lina maana sawa na neno lililopigiwa mstari katika sentensi hii?
A. Shwari C. Kushirikiana E. Ugomvi
B. Bahati D. Dharau

(vii) Neno lipi linajumuisha orodha ya maneno yafuatayo? kitumbua, andazi, mkate, chapati
A. Mlo C. Vitafunio E. Vitafunwa
B. Kifunguakinywa D. Vinywaji

(viii) Nimezaliwa mlimani nikafunikwa kwa majani jua likanipa joto daima nakwenda mbele siwezi kurudi nyuma. Je, fumbo hili hufumbuliwa kwa jibu lipi kati ya haya yafuatayo?
A. Moto C. Maji E. Dunia
B. Mwezi D. Jongoo

(ix) Kitendawili kipi kati ya hivi vifuatavyo huteguliwa kwa picha ifuatayo?



A. Akibeba watoto wake hawezi kuwashusha
B. Teketeke huzaa gumugumu na gumugumu huzaa teketeke
C. Huuawa na uzazi wake
D. Amefika kabla mjumbe hajarudi
E. Amesuka mkeka wake lakini bado analala chini.

(x) Nini maana ya nahau Nyota ya jaha?

A. Jua la mchana
B. Bahati
C. Nyota ya asubuhi
D. Bahati mbaya
E. Kuwa na aibu

3. Oanisha maelezo yaliyopo katika **Orodha A** na aina za maneno zilizopo katika **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika sehemu ya majibu

| Na | Orodha A | Majibu | Orodha B |
|---|---|---|---|
| (i) | Hutaja majina ya watu au mahali na mara zote huanza kwa herufi kubwa | (   ) | A. Nomino za dhahania |
| (ii) | Hutaja viumbe au hali kama vile mvulana, mtu, mama na wadudu | (   ) | B. Nomino za pekee |
| (iii) | Hutaja dhana za kufikirika tu ambazo hazionekani wala kushikika kama vile upendo, upepo, furaha na joto | (   ) | C. Nomino za jumla |
| (iv) | Hutaja vitu ambavyo viko katika makundi licha ya kwamba hutajwa kwa umoja kama vile kikosi, timu, kwaya, kundi na chama | (   ) | D. Nomino za kawaida |
| (v) | Husimama kama vibadala vya nomino | (   ) | E. Vitenzi |
| | | | F. Viwakilishi |
| | | | G. Vivumishi |

**SEHEMU B: (Alama 20)**

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii

4. Taja vinyume vya maneno yafuatayo kwa kuandika jibu katika nafasi iliyoachwa wazi.

(i) Ujinga______________________________________

(ii) Afiki______________________________________

(iii) Bandia______________________________________

(iv) Mchoyo______________________________________

(v) Adimika______________________________________

5. Soma kwa makini shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi katika sehemu iliyoachwa wazi

Yai, Kuku kwa maringo, wajidai hadharani,
Nani katika miongo, aliwahi duniani?
Nauliza wenye bongo, mliomo darasani,
Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

Chapuchapu lete jibu, nazo sababu nipeni,
Tuimalize sulubu, nyoyo ziwe na amani,
Tuwaondolee tabu, Yai, Kuku mzozoni,
Nani atutegulie, kitendawili cha jadi?

**Maswali**

(i) Shairi hili linahusu nini?

________________________________________

(ii) Shairi hili lina beti ngapi?

________________________________________

(iii) Andika kinyume cha neno 'hadharani' kama lilivyotumika katika mshororo wa kwanza wa ubeti wa kwanza

________________________________________

(iv) Neno 'miongo' kama lilivyotumika katika shairi hili lina maana gani?

________________________________________

(v) Katika ubeti wa kwanza mwandishi wa shairi hili anawauliza wenye bongo kuhusu nini?

________________________________________

**SEHEMU C: (Alama 10)**

Jibu swali la **sita (6)**

6. Kamilisha barua ifuatayo kwa kuchagua majibu sahihi kutoka kwenye kisanduku kisha uyaandike katika nafasi zilizoachwa wazi

| |
|---|
| **Yah: Ombi la kushiriki mchezo wa kirafiki , S.L.P. 256, Wako mtiifu, Mwalimu wa michezo, Ndugu, Daudi Kibona Shabani, Salaam sana,** |

Shule ya Msingi Kisoji,
(i).__________________
Vumbwe.
**20.02.2025**

Mwalimu Mkuu,
Shule ya Msingi Kisoji,
S.L.P 256,
Vumbwe.
(ii).__________________________
(iii)________________________________________
Tafadhali husika na kichwa cha habari hapo juu.

Mimi ni mwanafunzi wa Darasa la Sita. Ninaomba kwenda kushiriki mchezo wa kirafiki katika Shule ya Msingi Majengo. Mchezo huo utafanyika tarehe 21/02/2025 kuanzia saa 3:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana, katika viwanja vya shule hiyo.

Nitashukuru kama ombi langu litakubaliwa

(iv)____________________________________
D.K. Shabani
(v)_____________________________________